

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAJI**



TANGAZO LA NAFASI YA MWENYEKITI WA BODI YA MAJI YA TAIFA

Katibu Mkuu, Wizara ya Maji anatangaza nafasi ya Mwenyekiti wa Bodi ya Maji ya Taifa. Bodi hii inaundwa kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji Na. 11 ya mwaka 2009 chini ya Kifungu Na. 20. Muda wa Bodi ni miaka mitatu.

MAJUKUMU YA BODI YA MAJI YA TAIFA

- (a) Kuchunguza jambo lolote litakalowasilishwa kwake na Waziri au Wizara ya Sekta nyingine kuhusiana na usimamizi endelevu wa rasilimali za maji na kutoa mapendekezo yao kwa Waziri au Wizara ya Sekta husika, itakavyoona inafaa, kuchukua hatua madhubuti ili kufikia malengo ya Sheria hii;
- (b) Kushauri vipaumbele vya uwekezaji na mpangilio wa kifedha na kuratibu na kuunganisha miradi inayotekelezwa kwa fedha za nje na programu zenye kutoa mchango wa kuendeleza rasilimali za maji;
- (c) Kushauri katika kujumuisha mipango ya sekta mbalimbali kuhusu tathmini na kupanga rasilimali za maji;
- (d) Kushauri uratibu wa mipango ya bonde na usimamizi;
- (e) kushauri utatuzi wa migogoro kati ya sekta moja na nyingine na kati ya Bonde moja na lingine;
- (f) Kushauri vipaumbele vya uwekezaji na mpangilio wa kifedha;
- (g) Kushauri uhamisho wa maji baina ya mabonde;
- (h) Kushauri usimamizi wa rasilimali za maji shirikishi,
- (i) kupendekeza kwa Waziri hatua za kisheria kwa ajili ya usimamizi wa rasilimali za maji na njia madhubuti ya kuzuia uchafuzi wa maji;
- (j) Kushirikiana na Mkurugenzi kwenye masuala ya kiufundi;
- (k) Kuandaa taarifa ya kila nusu mwaka ya hali ya rasilimali za maji; na
- (l) Kutekeleza majukumu mengine ya kiushauri ya Sekta kama Waziri atakavyoona inafaa.

SIFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji wa nafasi hii anatakiwa kuwa na ujuzi na uzoefu katika masuala ya Sekta ya Maji au Sekta zinazohusiana na sekta hiyo. Awe na uzoefu na ujuzi katika masuala ya uongozi na usimamizi katika nyanja zinazohusiana na masuala ya usimamizi wa rasilimali za maji kwa muda usiopungua miaka 10. Aidha, awe na ujuzi mahsusi kwenye masuala ya usimamizi wa rasilimali za

maji na asiwe/ asitoke kwenye taasisi ambayo ni mtumiaji mkuu wa maji (Major Water User).

Maombi yatumwe kwa:

Katibu Mkuu,
Wizara ya Maji,
Mji wa Serikali,
Mtaa wa Maji,
S.L.P. 456,
40473, DODOMA.

Nakala ya maombi itumwe kupitia barua pepe: ps@maji.go.tz

Maombi yaambatishwe na wasifu wa mwombaji (CV) yenye wadhamini watatu na namba zao za simu. Andika “**Mwenyekiti Bodi ya Maji ya Taifa**” nyuma ya bahasha.

Mwisho wa kupokea maombi ni siku ya Ijumaa tarehe 15 Oktoba, 2021 saa 09.30 alasiri

Imetolewa na:

Katibu Mkuu
Wizara ya Maji
17 Septemba, 2021